TANZANIA HIGHER LEARNING INSTITUTIONS TRADE UNION
P.O. BOX **11727, DAR ES SALAAM**, Tanzania
Email: katibu@thtu.biz.tc, mtalo@thtu.biz.tc
Mobile: +255 755 576 224
Website: http://thtu.biz.tc

Tarehe: 12/03/2010

# TAMKO LA CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA (THTU) JUU YA DHAMIRA YA MGOMO WA WAFANYAKAZI WA SEKTA YA UMMA

Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU) kinapenda kuchukua fursa hii kuwaelezea wanachama wake na umma kwa ujumla msimamo wa Chama juu ya tamko la Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) kuhusu dhamira yao ya kuitisha mgomo wa Wafanyakazi nchi nzima tarehe 05/05/2010.

Ni ukweli usipingika kwamba madai yao ni ya msingi na yanagusa Wafanyakazi wote na pia ni ya muda mrefu. Tathmini inaonyesha kwamba matatizo hayo yamekuwa sugu na yamezidi kudumaza hali za Wafanyakazi.

Pamoja na hoja zao kuwa za msingi, suala la kujiuliza ni kwa kiasi gani Shirikisho (TUCTA) limekuwa likishiriki katika vyombo vya maamuzi na Serikali. Vyombo ambavyo vimeundwa hususani kwa ajili ya majadiliano ya uboreshaji wa hali za Wafanyakazi, Uchumi na sheria (LESCO) mathalani katika Tume ya Ntukamazina ambayo Mhe Rais aliiunda kwa ajili ya kujadili hali za Wafanyakazi na uboreshaji wa mishahara. TUCTA ilishiriki katika tume hii na matokea yake ni uundwaji wa bodi mbalimbali moja wapo ni bodi ya mishahara ya kisekta (Wage Board) ambapo mishahara hujadiliwa kwa kina na maamuzi hufikiwa.

Katika hoja ya sheria mbaya za kazi, TUCTA ilishiriki kikamilifu katika kuzitunga kama mdau muhimu.

Hali hii ya ushiriki wa TUCTA katika vyombo mbalimbali vya maamuzi na nia ya TUCTA kuandaa mgomo inaashiria kuwa kuna tatizo la msingi, aidha la mfumo wa ushirikishwaji wa Wafanyakazi ama ushiriki dhaifu katika vyombo vya maamuzi.

Kama tatizo ni mfumo, vyama viwe tayari kukataa mfumo huo kwa dhamira ya wazi kwa kujiondoa kwenye vyombo vya maamuzi, hili litakuwa ni fundisho kwa Serikali. Na iwapo tatizo ni udhaifu wa ushiriki wa vyama katika vyombo mbalimbali vya

maamuzi, ni vema vyama vijitathmini upya ili kuwa na ushiriki bora utakaoleta tija kwa Wafanyakazi.

Katika hali hii ni vema Serikali ione busara ya kutambua na kuheshimu madai ya Wafanyakazi na kuyapatia ufumbuzi wa haraka.

Pengine sasa ni wakati muafaka kwa Wafanyakazi kufanya tathmini ya kina katika mfumo wa ushirikishwaji na ushiriki wa vyama vyetu katika vyombo vya majadiliano na maamuzi ili kuleta tija na mabadiliko yanayotarajiwa.

Kwakuwa nia ya TUCTA ni kupata suluhisho la matatizo haya sugu ni dhahiri kwamba majadiliano ya kina yaliyofanyiwa upembuzi yakinifu ndio njia bora itakayowezesha kupatikana ufumbuzi wa kudumu wa matatizo haya. Silaha ya mgomo itakuwa na maana tu endapo majadiliano yatakuwa yameshindikana.

Kwa kuzingatia hoja hizi muhimu Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya juu Tanzania (THTU) hatuungi Mkono Mgomo huu kwa maslahi ya taifa.

**NIA NA MWELEKEO WETU DAIMA NI KUJENGA!**

K. S. Maswanya,

Katibu Mkuu, THTU